# SHERIA ZA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


### SEHEMU YA KWANZA
### UTANGULIZI

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.

### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009

2. Kusomwa.

3. Marekebisho ya kifungu cha 5.

4. Marekebisho ya kifungu cha 18.

5. Marekebisho ya kifungu cha 29.

6. Marekebisho ya kifungu cha 31.

7. Marekebisho ya kifungu cha 31A.

8. Marekebisho ya kifungu cha 57.

### SEHEMU YA TATU
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 7 YA 2017

9. Kusomwa.

10. Marekebisho ya kifungu cha 77.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI YA ZANZIBAR NAM. 1 YA 2006**

11. Kusomwa.

12. Kuongeza kifungu kipya cha 21A.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUTOZA KODI YA MAFUTA NAM. 7 YA 2001**

13. Kusomwa.

14. Kufuta kifungu cha 5.

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 11 YA 2004**

15. Kusomwa.

16. Marekebisho ya kifungu cha 19.

**SEHEMU YA SABA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO NAM. 1 YA 2003**

17. Kusomwa.

18. Marekebisho ya kifungu cha 2.

19. Marekebisho ya kifungu cha 4.

20. Kuongezwa Sehemu Mpya ya IIA.

**SEHEMU YA IIA**
**UZUWIAJI WA MAGENDO**

21. Kuongeza vifungu vipya vya 25A na 25B.

22. Marekebisho ya kifungu cha 31.

SEHEMU YA NANE
MAREKEBISHO YA SHERIA YA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR NAM. 10 YA 2017

23. Kusomwa.

24. Marekebisho ya kifungu cha 15.

**SHERIA NAMBA 9 YA 2018**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

3rd Julai, **2018**

# SHERIA ZA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato) ya 2018 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**3.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongeza maneno "ndani ya siku kumi na tano kuanzia tarehe ya kuanza biashara" mara tu baada ya neno "Kamishna".

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya kifungu cha 18. | **4.** Kifungu cha 18 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya kama ifuatavyo: |

"(2) Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika sheria mahsusi za kodi au kanuni, kila mlipa kodi analazimika, ndani au kabla ya siku ya ishirini ya kila mwezi kufuatia mwisho wa kipindi cha kufunga hesabu, kuandaa na kuwasilisha taarifa za kodi, ikiwa kodi imelipwa au haijalipwa katika kipindi hicho."

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya kifungu cha 29. | **5.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza kifungu kidogo kipya cha (7) mara tu baada ya kifungu kidogo kipya cha (6) kama ifuatavyo: |

"(7) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ushahidi, waraka wowote, kumbukumbu, kifaa cha kieletroniki au vitu mchanganyiko vinavyohusiana na hivyo au taarifa iliyopatikana kupitia kifaa cha kieletroniki au vitu mchanganyiko vinavyohusiana na hivyo kilichopatikana chini ya kifungu hiki kitakubalika kuwa ni ushahidi katika kesi yoyote dhidi ya mlipa kodi."

| | |
|---|---|
| Marekebisho ya kifungu cha 31. | **6.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: |

(a) kufuta aya (a) katika kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake aya ifuatayo:

"(a) isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika sheria au kanuni mahsusi za kodi, si zaidi ya siku ya ishirini ya mwezi kufuatia mwisho wa kipindi cha kufunga hesabu."

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara tu baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4)(a) Mlipa kodi anaweza, kwa maandishi, kuomba kwa Kamishna kuongezewa muda wa kulipa kodi katika Sheria ya kodi;

(b) Kamishna anaweza, baada ya kupokea maombi na ikiwa ataridhika kwamba kuna haja ya kuongezewa muda mlipa kodi kwa kutokuwepo Zanzibar, kuumwa au sababu nyengine ya msingi, kuongeza tarehe ambayo kodi au sehemu ya kodi itapasa kulipwa;

(c) Kamishna atampatia muombaji taarifa ya maandishi ya maamuzi kuhusiana na ombi lake; na

(d) Iwapo muda wa nyongeza umetolewa kwa kumruhusu mlipa kodi kulipa kodi kwa awamu na mlipa kodi akashindwa kulipa awamu yoyote, bakaa yote ya kodi inayostahiki kulipwa pamoja na riba italazimika kulipwa mara moja."

Marekebisho ya kifungu cha 31A.

**7.** Kifungu cha 31A cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta rejea "kifungu kidogo cha (1)" na kuweka badala yake "kifungu kidogo cha (2)".

Marekebisho ya kifungu cha 57.

**8.** Kifungu cha 57 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 57 kifuatacho:

"Kusamehe malipo ya faini au adhabu.

57(1) Waziri, kwa kushauriana na Kamishna, anaweza kusamehe kodi yote au sehemu ya kodi inayomstahiki mlipa kodi kuilipa kama itakavyoainishwa na kutangazwa katika Gazeti Rasmi na Waziri.

(2) Iwapo sababu ya msingi imetolewa kwa maandishi na mtu anaewajibika kulipa kodi chini ya Sheria hii, Kamishna anaweza, ikiwa ataona ni uwamuzi wa busara kuwa ni haki na ni sahihi kusamehe kodi yote au sehemu ya kodi hiyo, kutoa adhabu, riba au faini inayostahiki kulipwa chini ya Sheria hii, isipokuwa kwamba kama ni riba msamaha hautozidi asilimia hamsini ya jumla ya kiwango cha riba."

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU NAM. 7 YA 2017

Kusomwa.

**9.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 7 ya 2017 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 77.

**10.** Kifungu cha 77 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kifuatacho:

"(1) Kwa kuzingatia utaratibu utakaowekwa katika Kanuni chini ya Sheria hii, Waziri, kwa tangazo katika Gazeti Rasmi, anaweza kusamehe ushuru wowote unaotozwa chini ya Sheria hii itakapokuwa zipo sababu za kutosheleza kwa Maslahi ya Umma"

(b) kuingiza aya mpya (c) katika kifungu kidogo cha (2):

"(c) Hati yoyote inayohaulisha mali isiyohamishika ikijumuisha ardhi na majengo bila ya malipo au kutoa kitu chengine cha thamani kwa ajili hiyo katika mirathi, au baina ya mzazi au mlezi kisheria na mtoto;"

(c) kufuta kifungu kidogo cha (3) na kuingiza badala yake kifungu kidogo kipya cha (3)":

"(3) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ushuru hautalipwa na wafuatao:

(a) Mradi wowote ulioidhinishwa chini ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar, iwapo msamaha umetolewa chini ya Sheria hiyo; na

(b) Mashirika ya ndege yanayotoa tiketi za usafiri wa kimataifa."

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA RUFAA ZA KODI YA ZANZIBAR NAM. 1 YA 2006

Kusomwa.

**11.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Rufaa za Kodi ya Zanzibar Nam. 1 ya 2006 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 21A.

**12.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 21A kama ifuatavyo:

"Uwezo wa Bodi au Baraza katika utaratibu.

21A (1) Katika kuendesha shauri lolote mbele ya Bodi au Baraza, utaratibu wa Bodi au Baraza, kwa mujibu wa Sheria hii na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, utakuwa ndani ya mamlaka ya Bodi au Baraza kwa mujibu wa hali itakavyokuwa.

(2) Mwenendo wa shauri lolote mbele ya Bodi au Baraza utaendeshwa kwa utaratibu rasmi na wa kiufundi ulio mdogo kwa kadri inavyowezekana na Bodi au Baraza halitolazimika kufuata kanuni za ushahidi lakini linaweza kujiridhisha kwa jambo lolote namna ambayo itaona inafaa.

(3) Iwapo Sheria na kanuni zilizowekwa chini ya Sheria hii hazijaeleza kuhusiana na mwenendo wowote mahsusi au

utaratibu, utaratibu wa Bodi au Baraza utaendeshwa kwa mujibu wa mwenendo wa kanuni na taratibu ambazo kwa kawaida hufuatwa kama Bodi au Baraza litakavyoainisha."

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUTOZA KODI YA MAFUTA NAM. 7 YA 2001

Kusomwa.

**13.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kutoza Kodi ya Mafuta Nam. 7 ya 2001 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta kifungu cha 5.

**14.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinafutwa.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UKUZAJI NA KULINDA VITEGA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 11 YA 2004

Kusomwa.

**15.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ukuzaji na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar Nam. 11 ya 2004 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**16.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "wakati wa kipindi cha ujenzi" yanayojitokeza baina ya neno "ardhi" na "mkakati" chini ya kifungu kidogo cha (2);

(b) Kufuta "*proviso*" chini ya kifungu kidogo cha (2);

(c) Kuingiza kifungu kidogo kipya cha (3) mara tu baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

> "(3) Muda wa msamaha chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki utakuwa kama itakavyoelezwa kwenye Jadweli la Kwanza la Sheria hii."

(d) Kukipa namba upya kifungu kidogo cha (3) kilichokuwepo kuwa kifungu kidogo cha (4) kwa mpangilio wake.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO NAM. 1 YA 2003

Kusomwa.

**17.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya 2003 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**18.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta tafsiri ya maneno "magendo", "Ofisa" na" baharia" na kuweka badala yake tafsiri mpya ya maneno hayo kwa mpangilio wake:

"Magendo" maana yake ni kuingiza, kusafirisha, au kusafirisha katika mwambao au usafirishaji, au uondoshaji ndani au nje ya Zanzibar, bidhaa, vitu, au bidhaa nyengine yoyote kinyume cha sheria kwa lengo la kukosesha mapato, au kuepuka marufuku ya, vikwazo juu ya, kanuni au masharti yanayohusiana na uingizaji huo, usafirishaji huo, kusafirisha katika mwambao huko, kusafirisha au kuondoa";

"Ofisa" maana yake ni askari wa KMKM mwenye cheo kilicho juu ya cheo cha baharia";

"Baharia" maana yake ni askari wa KMKM mwenye cheo kilicho chini ya cheo cha Ofisa".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**19.** Kifungu cha 4 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) Kuongeza maneno "au baharia" mara tu baada ya neno "Ofisa" lililopo katika kifungu kidogo cha (2);

(b) Kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara tu baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Taratibu za ukamataji, upekuzi, na utafutaji mpaka kufikia kukabidhi utaelezwa katika Kanuni na pale ambapo hakuna Kanuni taratibu zilizoelezwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai zitatumika."

Kuongezwa Sehemu Mpya ya IIA.

**20.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza Sehemu IIA mara tu baada ya Sehemu ya II kama ifuatavyo:

## SEHEMU YA IIA
## UZUWIAJI WA MAGENDO

Uwezo wa KMKM wa kuzuwia magendo.

4A (1) Bila kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, KMKM itakuwa na uwezo na mamlaka ya kuzuwia magendo.

(2) Katika kutumia uwezo na mamlaka yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo (1):

(a) Ofisa au baharia wakati akiwa kazini anaweza kuingia, kufanya doria na kuingia bila vikwazo ndani ya chombo cha usafiri baharini, gari na eneo lolote lisilokuwa nyumba ya kuishi.

(b) Ofisa au baharia anaweza, kuingia na kupekuwa ndege yoyote, chombo cha usafiri baharini au gari na anaweza kuchunguza, kufunga, kuziba, kuweka alama au vyenginevyo kuweka katika mazingira salama, bidhaa yoyote katika ndege hiyo, gari au chombo cha usafiri baharini, na kwa madhumuni ya kuchunguza au usalama wa bidhaa yoyote, ofisa au baharia huyo anaweza kutaka bidhaa hizo zishushwe, au zitolewe kwa gharama za mweye ndege, chombo cha usafiri baharini au gari.

(c) Ofisa au baharia chini ya kifungu hiki ambaye hakuweza kuingia bila vikwazo sehemu yoyote ya ndege hiyo, gari, chombo cha usafiri baharini, au kontena lolote, anaweza kuingia sehemu hiyo, au anaweza kuingia katika sehemu hiyo, au kufungua kontena hilo, katika hali ambayo, ikibidi kwa kutumia nguvu kwa kadiri atakavyoona inamlazimu.

(d) Mtu ambaye anamzuwia ofisa kuweza kuingia bila vikwazo anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kutumikia kifungo kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitano.

(3) Ofisa au baharia wakati wa kutekeleza majukumu yake anaweza, mbali na kutumia uwezo aliopewa katika kuzuwia magendo chini ya Sheria hii, kutumia uwezo na kufuata taratibu walizopewa maafisa chini ya Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Forodha pamoja na Kanuni zake.

Kuongeza vifungu vipya vya 25A na 25B.

**21.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 25A na 25B mara tu baada ya kifungu cha 25 kama ifuatavyo:

"makosa yanayo-husiana na magendo.

25A (1) Mtu anayefanya magendo anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kwa adhabu zote zifuatazo:

(a) kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba lakini kisichozidi miaka ishirini na tano;

(b) kulipa faini sawa na thamani ya wanyama, bidhaa, vitu au bidhaa nyengine ambazo alidhamiria kusafirisha, kuingiza, kuondosha au kuchukua;

(c) gari yoyote, chombo cha usafiri baharini, ndege au kitu chengine chochote kilichotumika kwa kusafirishia au kilichokuwa kitumike kusafirishia watu hao, wanyama, bidhaa, vitu au bidhaa nyengine, vitataifishwa na Serikali bila kujali kama gari hiyo, chombo cha usafiri baharini, ndege au kitu chengine kuwa ni miliki ya mtuhumiwa au la; na

(d) bidhaa yoyote inayohusiana na kosa la magendo itataifishwa.

(2) Iwapo chombo cha usafiri baharini, au ndege ni ya kigeni itazuiliwa hadi yafanyike malipo kwa fedha za kigeni zilizo sawa na Milioni Ishirini kwa Shilingi za Kitanzania.

(3) Iwapo gari, chombo cha usafiri baharini, ndege, au kitu chengine chochote kilichotumika au kilikuwa kitumike kwa kusafirishia bidhaa hizo muhimu au zilizodhibitiwa kinamilikiwa na Serikali au mashirika yake, dereva au mtu mwengine yeyote aliyepewa dhamana ya gari hiyo, chombo cha usafiri baharini, ndege, au kitu chengine kwa kadiri itakavyokuwa na au mtu ambaye amemuidhinisha dereva huyo au mtu huyo atalazimika kulipa faini ya kiwango cha thamani ya wanyama, bidhaa, vitu au bidhaa nyengine alizokusudia kusafirisha, kuingiza, kuondosha au kuchukua, au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitano."

"anaesaidia na kuchangia.

**25B**. Mtu yeyote anaesaidia, anaechangia, anaeficha au kuwezesha kutendeka kwa kosa la magendo atachukuliwa sawa na kuwa amefanya kosa la magendo na atakuwa ni mkosa wa kosa la magendo."

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**22.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongeza aya mpya ya (h) mara tu baada ya aya ya (g) na kuipa nambari upya aya (h) kuwa (i) kwa mpangilio wake:

"(h) zawadi zinazowezekana kupewa kwa maafisa au watu waliosaidia katika kufanikisha ukamataji wa mtu yeyote aliyetuhumiwa na kuthibitishwa kufanya kosa la magendo."

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR NAM. 10 YA 2017

Kusomwa.

**23.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar Nambari 10 ya 2017 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**24.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) (a) na kuandikwa upya kifungu kidogo cha (1) (a) kama ifuatavyo:

"15(1)(a). Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, ambae atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi na Katibu Mkuu wa Baraza."

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 27 Juni, 2018.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***